JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

APRLIL 20, 2025 | ISSUE NO 13

Multisectoral magazine



## RAIS SAMIA
### KINARA WA MAPINDUZI
### JIKONI

80

Mkakati huo una lengo la kuhakikisha kuwa asilimia ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034

## MATUMIZI nishati *safi*
## UHAI WA MWANAMKE TANZANIA

TSHS.20,000 KSHS.1,187 USHS 30,000
ISSN 2799-225X | LESENI 00000021
www.tz&beyond.co.tz

**469,000**
HEKTA ZA MISITU KUOKOLEWA KWA MWAKA

**MAZINGIRA**
VYANZO VYA MAJI KUWA SALAMA, MVUA KUWA ZA UHAKIKA,NCHI KUWA NA KILIMO CHENYE TIJA

**33,000**
KUEPUKANA NA VIFO VINAVYOSABABISHWA NA MOSHI WA KUNI NA MKAA

**IMAGINE YOUR LIFE WITHOUT YOUR EYES...**

VISION PLUS
the eye clinic



MIKOCHENI (SHOPPERS PLAZA) |
AFYA HOUSE | CITY CENTER (SAMORA TOWERS)
| ZANZIBAR - AIRPORT ROAD

+255 778 227 252

hwd@visionplustz.com


# BODI YA WAHARIRI


**AFISA MTENDAJI MKUU**
JIMMY C. KIANGO
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MHARIRI MTENDAJI**
JIMMY C. KIANGO
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MHARIRI:**
SIDI MGUMIA
Cell: 0714327572
mgumia.sidi@tz&beyond.co.tz

**MENEJA WA IT**
FELIX JIMMY ALOYCE
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MSANIFU KURASA MKUU**
FELIX JIMMY ALOYCE
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MWANDISHI**
HASSAN DAUD
**Cell: 0692 695 889**
hassan.@tz&beyond.co.tz

**MWENYEKITI**
DK. THOMAS KASHILILAH
[FCLPP, CIPM,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
legiconsult@outlook.com

**MLEZI**
NASSIR ABDALLAH
Cell: 0713 767685
nasir.abdallah@panaromanews.co.tz



**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania

**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com





www.tz&beyond.co.tz






21
MTUE MAMA MZIGO WA KUNI, TUNZA MAZINGIRA


28
MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA NI AGENDA MAHSUSI


08
RAIS SAMIA NA MAMBO MATATU


45
KAULI ZA WABUNGE NISHATI SAFI YA KUPIKIA


31
LENGO LA SERIKALI ASILIMIA 80 KUTUMIA NISHATI SAFI


12
UMUHIMU WA KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA


10
KAULI ZA WABUNGE NISHATI SAFI YA KUPIKIA


14
6.7% NDIO WANATUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA


24
AMEBORESHA HUDUMA YA AFYA KWA MAMA NA MTOTO


09
MATUMIZI YA NISHATI ISIYO SAFI KATIKA KUPIKIA INAUA WATANZANIA 33,000 KILA MWAKA


17
KILA TANZANIA KUINGIA KATIKA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

# TZ&BEYOND




***Jarida hili linalowafikia watu wa rika na kada*** mbalimbali ndani na nje ya Tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.

**TZ&BEYOND** limejikita kwenye kuchambua masuala ya siasa, Bunge, Uchumi, Mazingira, Uhifadhi na Habari za kimataifa dhamira yake kuu ni kuwa darasa mikononi mwako.

***TUNA MWANZO, HATUNA MWISHO***

USIKOSE KUSOMA MAJARIDA YETU KUPITIA TOVUTI

www.tz&beyond.co.tz




JICHO LA TZ&BEYOND



# MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA NI AGENDA MAHSUSI

*Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikibuni na kutekeleza Sera na mikakati yenye lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati sa¦ ya kupikia pamoja na utunzaji wa mazingira.*

Matumizi ya nishati safi ya kupikia ni agenda mahususi ambayo imechukua nafasi kubwa katika Sera, mipango na mikakati ya serikali mbalimbali duniani.

Umuhimu wa agenda hii unasukumwa na ongezeko la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na athari za kiafya zinzotokana na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Lengo Namba 7 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa limejikita katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati nafuu, inayopatikana kwa urahisi, endelevu na ya kisasa kwa wote.

Hata hivyo bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa nishati nafuu, endelevu na za uhakika kwa ajili ya matumizi mbalimbali hususan ya kupikia hasa kwa nchi zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania.

Hali hii inasababisha wananchi wengi na baadhi ya taasisi kuendelea kutumia nishati isiyo safi ya kupikia, jambo linaloendelea kuchochea ongezeko la athari za kimazingira, kiafya, kiuchumi na kijamii.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikibuni na kutekeleza Sera na mikakati yenye lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na utunzaji wa mazingira.

Pamoja na utekelezaji wa Sera na mikakati hiyo chini ya sekta na taasisi mbalimbali, hakuna mwongozo wa Kitaifa unaotoa nishati safi ya kupikia na kuondokana na nishati chafu.

Kutokana na hali hii, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa Mjadala wa Kitaifa wa Nishati safi ya kupikia mwaka 2022 alielekeza kuangaliwa kwa Mkakati wa Taifa utakaotoa mwongozo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Kwa muktadha huo, serikali imeandaa mkakati wa taifa wa Matumizi ya nishati safi ya kupikia ambao unatoa mwelekeo wan chi wa kuhamia katika nishati safi ya kupikia.

Mkakati huo una lengo la kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Hivyo natumia fursa hii kutoa wito kwa wadau wote, zikiwemo Wizara za kisekta, Taasisi za umma, Idara za Serikali, Tawala za Miko ana serikali za Mitaa, asasi za kiraia, sekta binafsi, washirika wa maendeleo na umma kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mkakati huu.

Ni imani yangu kuwa ifikapo mwaka 2034 nchi yetu itakuwa imepiga hatua kubwa kayika kukuza kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia, hali itakayowezesha utunzaji wa mazingira, kuboresha afya na ustawi wa jamii, kukuza uchumi na kuchangia kufikiwa kwa Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030.

MTUE MAMA KUNI MAMA

RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN NI SHUJAA NA MWOKOZI WA MWANAMKE JIKONI, NI YEYE NDIE ALIEAMUA KULIBEBA JUKUMU LA KUMUOKOA MWANAMKE NA ADHA YA MATUMIZI YASIYO FAA JIKONI.



# Rais samia na MAMBO matatu









NA MWANDISHI WETU

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni shujaa na mwokozi wa mwanamke jikoni, ni yeye ndie alieamua kulibeba jukumu la kumuokoa mwanamke na adha ya matumizi yasiyo faa jikoni.

Ikumbukwe kuwa matumizi ya nishati isiyo safi katika kupikia inaua Watanzania 33,000 kila mwaka kutoka na moshi wa kuni na mkaa, aidha hekta za misitu 469,000 zinakatwa kila mwaka.

Hii ni hatari na inaweza kuliangamiza taifa kutokana na kasi ya mabadiliko ya tabia nchi, hatua hii imemfanya Rais Dkt. Samia kulibeba jambo hili kwa nguvu zake zote.

Rais Dkt. Samia amelibeba jambo hili si kwa Tanzania pekee bali Afrika kwa ujumla, Mei 14,2024 akiwa nchini Ufaransa kwenye mkutano wa Kimataifa wa Nishati ya Kupikia ambapo pia alikuwa ni Mwenyekiti mwenza wa mkutano huo alisema matumizi ya nishati safi yanasaidia kulinda afya na kuokoa muda kwa wanawake waliokuwa wanatafuta kuni.

Alisema zaidi ya Waafrika milioni 900 wanatumia nishati ya kupikia isiyo safi jambo linalochangia kuharibu

# Nishati safi ya

## KUPIKIA UHAI WA *Mwanamke*

Maisha ya wanawake wengi wa mijini na vijijini yanatajwa kuwa hatarini kutokana na wengi wao kutumia kuni na mkaa kupikia chakula.

Ni asilimia 6.9 tu ya Watanzania wote ndio wanaotumia nishati safi ya kupikia, walio salia wote wanatumia nishati isiyo safi, hii ni hatari kwa uhai wa mwanamke. Hata hivyo dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwa kinara wa nishati safi ya kupikia, inatazamwa kama mpango mpya wenye lengo la kumtua mama mzigo wa kuni na kumuondolea adha za kiafya.

Nishati safi ya kupikia hupimwa kwa ufanisi, urahisi wa kutumia, upatikanaji, usalama, unafuu na yenye kiwango kidogo cha sumu. Hii ni kwa mujibu wa mwongozo wa Benki ya Dunia kuhusu nishati safi ya kupikia (World Bank Multi-Tier Frame work-MTF) wa mwaka 2020.

Aidha mwongozo wa Shirika la Afya Duniani wa mwaka 2021 umeeleza kuwa nishati safi na teknolojia hupimwa kwa viwango vya chembechembe ndogi za vumbi zenye ukubwa usiozidi 2.5um (PM2.5) na hewa ya kaboni monoksiidi zinatolewa. Kwa Tanzania mkakati wa nishati safi ya kupikia ni dhana inayotumika kuelezea na kubainisha nishati na teknolojia sahihi ambapo kwa pamoja hutoa moshi wenye kiwango kidogo cha sumu pale zinapotumika kwa usahihi.

Dhana hii ina lengo la kuhakikisha usalama, uendelevu na urahisi wa upatikanaji wa nishati ya kupikia kuokoa muda, pamoja na kupunguza gharama za matumizi, athari za kimazingira na kiafya kwa watumiaji.

Aidha ni nyenzo muhimu katika kutekeleza makubaliano ya kitaifa na kimataifa yanayolenga kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji wa gesi joto. Mkakati wa taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia unatokana na hitaji la kuwa na mpango jumuishi wa kitaifa katika kukabiliana na ongezeko la uharibifu wa mazingira pamoja na athari za kiafya, kiuchumi na kijamii zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia.

Kutokana na suala la nishati ya kupikia kuwa mtambuka,kumekuwa na changamoto ya utekelezaji wa mikakati ya kupunguza athari hizo. Tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961 haijawahi kuwa na mpango jumuishi wa kitaifa wa kupunguza matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia. Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 imeeleza kuwa ongezeko la matumizi ya nishati ya tungamotaka pamoja na teknolojia zisizo fanisi za kupikia, namna za matumizi ya nishati katika kupika na matumizi ya majiko yasiyo fanisi imechangia katika uharibifu wa mazingira na matatizo ya kiafya yanayohusiana na moshi.

Hivyo ni muhimu kutekeleza jitihada za kuhamia katka matumizi ya nishati nyengine kama vile gesi asilia, gesi oevu (LPG) na umeme. Mkakati umeandaliwa ili kutekeleza lengo la sera ya taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 la kuboresha maisha ya wananchi kupitia matumizi ya nishati za kisasa za kupikia pamoja na matamko ya kisera kwa kuimarisha mabadiliko ya nishati ya kupikia kutoka kwenye kuni na mkaa kwenda kwenye nishati za kisasa na kuwezesha matumizi ya majiko na vifaa sahihi vya kupikia ili kukuza matumizi ya nishati safi za kupikia ambazo ni mbadala wa kuni na mkaa.

Utekelezaji wa mkakati utawezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa katika sera mbalimbali za kitaifa ikiwemo sera ya taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 yenye lengo la kuimarisha uhifadhi wa misitu kwa ajili ya utunzaji wa mazingira kupitia matumizi ya nishati mbadala zenye gharama nafuu na zinazopatikana kwa urahisi kama vyanzo vya nishati ya kupikia.

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 yenye lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mazao na huduma za misitu kwa kudumisha eneo la misitu la kutosha chini ya usimamizi Madhubuti. Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007 inayoelekeza kuwa utaratibu mzuri na endelevu wa kuhifadhi, kutunza na kulinda mazingira kwa faida ya afya ya wananchi wa vizazi vijavyo na sera ya taifa ya Maendeleo ya mwanamke na jinsia ya mwaka 2000 inayolenga kutunza mazingira kwa ajili ya kumpunguzia mwanamke mzigo wa kutafuta kuni na maji ili kuwezesha ushiriki wake katika kutekeleza shughuli za kijamii.

> KWA MUJIBU WA TAKWIMU ZA BENKI YA DUNIA ZA MWAKA 2023 IDADI YA WATANZANIA WANAOUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA IMEKUWA IKIONGEZEKA KWA KIWANGO KIDOGO KUTOKA ASILIMIA 1.5 MWAKA 2010 HADI ASILIMIA 6.9 MWAKA 2021.






# ...nishati safi ya KUPIKIA

Kuna kila sababu kwa Tanzania kuingia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na wataalamu wanasema kuwa tumechelewa.

MTUE MA KUNI MA

> Takribani asilimia 90 ya kaya nchini hutumia nishati ya kuni na mkaa kama nishati kuu ya kupikia, ambapo matumizi ya kuni ni asilimia 63.5 na mkaa ni asilimia 26.2, asilimia 10 zilizobaki zinajumuisha asilimia 5.1 ya LPG, asilimia 3 ni umeme na asilimia 2.2 ni nishati nyengine.

Wakati wa ufunguzi wa mjadala wa kitaifa wa Nishati safi ya kupikia uliofanyika Novemba 2022, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alielekeza kuandaliwa kwa mkakati wa taifa wa Nishati safi ya kupikia utakaotoa mwelekeo wa namna ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Aidha Rais alielekeza kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wawe wamehamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia ndani ya kipindi cha miaka 10.

Madhamuni ya mkakati wa kitaifa ni kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, salama, nafuu ya kupikia inakuwa endelevu na ya uhakika.

## NISHATI INAYOTUMIKA SASA

Nishati na teknolojia zinazotambulika kuwa safi kwa matumizi kutokana na kuwa na kiwango kidogo cha sumu ni pamoja na umeme, bayogesi, gesi asilia, LPG, bayoethano, nishati ya jua, majiko banifu na mkaa mbadala wenye viwango vilivyothibitishwa na mamlaka ya kudhibiti viwango.

Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2023 idadi ya Watanzania wanaoutumia nishati safi ya kupikia imekuwa ikiongezeka kwa kiwango kidogo kutoka asilimia 1.5 mwaka 2010 hadi asilimia 6.9 mwaka 2021.

Kiwango hiki ni chini ya kiwango cha wastani cha dunia cha asilimia 71 kwa mwaka 2021.

Nishati na teknolojia zinazotumika nchini kwa ajili ya kupikia ni pamoja na kinyesi cha wanyama na mabadi ya mimea, kuni, mkaa, mafuta ya taa, mkaa mbadala, bayoethano, LPG,gesi asilia, bayogesi, umeme, majiko banifu na majiko ya nishati ya jua.

Kwa mujibu wa cooking Rnergy Action Plan ya mwaka 2022 ilionesha kuwa asilimia 82 ya nishati kuu inayotumika nchini inatokana na tungamotaka (biomass). Kwa matumizi ya kupikia inakadiriwa kuwa takribani asilimia 90 ya kaya nchini hutumia nishati ya kuni na mkaa kama nishati kuu ya kupikia, ambapo matumizi ya kuni ni asilimia 63.5 na mkaa ni asilimia 26.2, asilimia 10 zilizobaki zinajumuisha asilimia 5.1 ya LPG, asilimia 3 ni umeme na asilimia 2.2 ni nishati nyengine.

## UMUHIMU WA KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

Kwa hali ilivyo sasa kuna kila sababu kwa Tanzania kuingia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na wataalamu wanasema kuwa tumechelewa.

Matumizi ya nishati safi ya kupikia, yatatuondoa kwenye athari za kiafya, kimazingira, kiuchumi, kielimu pamja na kijamii.

## AFYA

Moshi unaotokana na matumizi ya nishati isiyo safi huwa na gesi zenye sumu pamoja na chembechembe ndogo za vumbi zenye viambato vya sumu ambazo huweza kudhoofisha mfumo wa upumuaji na kusababisha magonjwa sugu kama kikohozi, homa ya mapafu, kifua kikuu, pumu na saratani ya mapafu.

Aidha sumu hizo husababisha kuharibika kwa ujauzito, kujifungua kabla ya wakati au kujifungua watoto wenye matatizo kiafya.

Magonjwa mengine yanayohusishwa na sumu hizo ni pamoja na magonjwa ya moyo na macho, shinikizo la dam una kupooza.

Waathirika wakubwa wa matatizo haya ya kiafya ni watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na wanawake ambao hutumia muda mwingi jikoni kuandaa chakula.

Ubebaji wa mizigo mikubwa ya kuni migongoni au vichwani huathiri uti wa mgongo, kichwa na miguu ya wanawake na watoto.

Athari hizi za kiafya husababisha kuelemewa kwa mifumo ya afya kutokana na magonjwa ambayo yangeweza kuepukika kama nishati safi za kupikia zingetumika.











MKAKATI HUU ULIOZINDULIWA NA RAIS SAMIA MEI 8,2024

UMELENGA KUPUNGUZA NA PENGINE KUONDOA KABISA UKATAJI WA MITI

# WATANZANIA 6.7% NDIO WANATUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

NISHATI SAFI YA KUPIKIA INA MAENEO MATATU YANAYOLIFANYA JAMBO HILO KUKABILIWA NA MKWAMO

baadhi ya watu kutolipatia suala la niashati safi ya kupikia kipaumbele.

uwezo mdogo wa kiuchumi wa watu wa vijijini kutokana na gharama kubwa ya upatikanaji wake.

kutokuwepo kwa ushirikiano wa kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kiurahisi.

watumiaji wa nishati safi ya kupikia nchini ni asilimia 6.7,

kutokuwepo kwa ushirikiano wa kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kiurahisi.









> Katika kufanikisha mkakati huo serikali imeanza kazi ya kugawa mitungi 70,000 ya gesi na bado kuna uhitaji mkubwa na kwamba wataongeza mitungi ya gesi 200, na kwamba wametoa nafasi kwa sekta binafsi kusaidia kufikia malengo hayo.

NA JIMMY KIANGO

Tanzania imeingia kwenye mkakati wa kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia mbinu mbalimbali, miongoni mwa mbinu hizo ni kuzindua mkakati wa Nishati safi ya kupikia.

Mkakati huu uliozinduliwa na RaisDkt. Samia Suluhu Hassan, Mei 8,2024, jijini Dar es Salaam, umelenga kupunguza na pengine kuondoa kabisa ukataji wa miti kwenye mapori na misitu mbalimbali nchini. Kwa sasa nchini Tanzania nishati safi ya kupikia ndio inatazamwa kuwa mwokozi katika utunzaji wa mazingira, takwimu zinaonesha kuwa idadi kubwa ya Watanzania wanatumia nishati chafu ya kupikia kama vile kuni na mkaa.

Asilimi 6.7 ambayo ni sawa na Watanzania wasiozidi milioni tano kati ya Watanzania zaidi ya milioni 61 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 ndio wanatumia nishati safi ya kupikia.

Takwimu hizo si nzuri na ndipo serikali ilipoamua kuweka lengo la kuhakikisha hadi kufikia mwaka 2034 idadi ya watumiaji wa nishati safi ya kupikia nchini inafikia asilimia 80, ambayo ni zaidi ya Watanzania milioni 48.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Dotto Biteko amesema wazi kuwa Tanzania bado iko nyuma katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Dkt. Biteko amekiri kuwa ni kweli watumiaji wa nishati safi ya kupikia nchini ni asilimia 6.7, tukizidiwa na jirani zetu wa Kenya ambao wamefikia asilimia 23 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.





# 6.7% NDIO WANATUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

MTUE KUNI MAMA

Inakadiriwa kuwa utafutaji wa kuni hasa vijijini hutumia wastani wa saa sita kila siku hali ambayo inaathiri shughuli za kiuchumi kutokana na kutumia muda mrefu kutafuta nishati hiyo




“Hali tuliyonayo kwa matumizi ya nishati safi ya kupikia ni asilimia 6.7 kwa sasa ukilinganisha na wenzetu wa Kenya wao ni asilimia 23, Uganda asilimia 0.7, Ghana asilimia 30 na waliopiga hatua zaidi katika matumizi ya Nishati safi ya kupikia kwa watu wao ni India yenye asilimia 71.7.”alisema.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO**

Dkt. Biteko amesema changamoto iliyopo kwa sasa katika eneo la nishati hiyo ni gharama, elimu ya nishati safi kutokuwepo na uwekezaji mdogo.

Alisema katika kuhakikisha changamoto hizo zinatatuliwa serikali imeandaa mkakati wa nishati safi ya kupikia ili ifikapo mwaka 2034 watumiaji wafikie asilimia 80 huku gharama ya utekelezaji wa mkakati huo ikiwa sh. trilioni nne.

Dkt. Biteko alisema mkakati huo utawezesha kutatua changamoto hizo kwa kuhakikisha upatikanaji wake unakuwa wa kutosha katika kila eneo la nchi kwa kuweka vituo vidogo katika kila kata ili kuwawezesha watu kujaza gesi kwa bei rahisi na kuwawekea mazingira wezeshi wawekezaji pamoja na kutoa elimu juu ya nishati safi ya kupikia kwa Watanzania wengi zaidi.

Katika kufanikisha mkakati huo serikali imeanza kazi ya kugawa mitungi 70,000 ya gesi na bado kuna uhitaji mkubwa na kwamba wataongeza mitungi ya gesi 200, na kwamba wametoa nafasi kwa sekta binafsi kusaidia kufikia malengo hayo.

Aidha serikali imekaribisha teknolojia itakayosaidia ujazaji wa gesi unaoendana na mahitaji ya mtumiaji kulingana na fedha aliyonayo.

“Matumizi ya gesi asilia ni jambo jipya nchini linalohitaji uwekezaji mkubwa hivyo watu wengi wamekuwa hawataki kuwekeza kwa sababu limekuwa likihitaji kutumia fedha nyingi ambazo matokeo yake ni ya muda mrefu.

“Hali hiyo inawafanya watu wanaowekeza kuwa ni wachache na baada ya kutokea maneno kuwa hiyo gesi haitatumika kwa muda mrefu watu wengi waliacha kuwekeza, lakini tayari wapo wawekezaji walioamua kujitokeza.”

Kwa mujibu wa taarifa kutoka wizara ya Nishati ni kuwa mara ya mwisho kwa serikali kutoa leseni ya kuendeleza vitalu vya gesi ilikuwa ni mwaka 2006, tangu hapo hakujawahi kutolewa leseni nyengine.

# 6.7% NDIO

## WANATUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

Gesi inayozalishwa sasa inatumika kwa matumizi ya umeme kwa asilimia 80, huku matumizi ya ndani yakiwa madogo kwa sababu usafirishaji wake unahitaji uwekezaji mkubwa unaohusisha usambazaji wa mabomba maalum majumbani.

Hata hivyo Dkt. Biteko amesema serikali ya awamu ya Sita imeamua kuendeleza kitalu cha Ntolia ambacho kitatoa futi za ujazo milioni 140 kwa siku na Baraza la Mawaziri limeidhinisha kutolewa kwa leseni na hiyo ambayo itakuwa ya kwanza kutolewa tangu mwaka 2006.

"Tayari sasa wawekezaji wengi wamejitokeza kuna vituo vya kujaza gesi vichache, sasa serikali imetoa leseni sita za kujenga vituo vya kujaza gesi katika magari na sasa inaanza kuongeza upelekaji gesi katika nyumba za watu kwa mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Mtwara huku zaidi ya nyumba 1500 zitaendelea kuunganishwa na gesi asilia.



Kuna kila sababu kwa Tanzania kuingia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na wataalamu wanasema kuwa tumechelewa.











# TPDC NAUTEKELEZAJI WA MKAKATI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

NA MWANDISHI WETU

SERIKALI imeoneshwa kuridhishwa na kazi inayofanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) ya kuwaunganishia wananchi gesi asilia kutoka kwenye bomba kuu.

Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango ameyasema hayo wakati wa kukagua mabanda kwenye Kongamano la Wanawake la Nishati safi ya kupikia, ambapo amesema shirika hilo linafanya kazi nzuri ambayo itachangia wananchi kuachana na nishati chafu ya kupikia.

Dkt. Mpango amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo Mussa Makame kuhakikisha wanaendelea kusambaza gesi asilia kwa wananchi huku akilitaka shirika hilo liangalie uwezekano wa njia za kupata pesa zaidi kwa ajili kuongeza nguvu katika utekelezaji wa majukumu yake.

Aidha Makame amesema shirika hilo limeanza safari ya kuwezesha wananchi wa Mikoa ya Lindi,Mtwara,Pwani na Dar es Salaam kutumia gesi asilia inayozalishwa hapa nchini. Makame amesema mpaka sasa wameshaunganisha takriban taasisi 13 yakiwemo baadhi ya magereza na shule na wameunganishia wananchi 1500.

Hata hivyo Mkurugenzi huyo amesema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni usambazaji wa gesi kwa bomba njia ambayo gharama yake ni kubwa huku akisema wanaangalia uwezekano wa kusambaza gesi asilia kwa njia ya mitungi ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kuhama kwenye matumizi ya kuni na mkaa na badala yake waanze kutumia nishati safi ya kupikia. TPDC ni kampuni ya mafuta ghafi (petroli) ya kitaifa ya Tanzania inayomiliki leseni zote za maendeleo ya vyanzo vya mafuta na gesi nchini.

Kampuni hii ilianzishwa kupitia Tangazo la Serikali Na.140 la Mei 30,1969 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na.17 ya mwaka 1969. Shirika lilianza kufanya kazi mwaka1973 na ni shirika la serikali inayomilikiwa kikamilifu na hisa zake zote zikiwa na Msajili wa Hazina. Mwaka 2015 Bunge la Tanzania lilipitisha sheria zinazohusu mafuta na kazi ya kampuni hiyo, Sheria ya Mafuta ya 2015, Sheria ya Sekta ya Uziduaji Tanzania (Uwazi na Uwajibikaji) ya 2015, na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya 2015.

Makadirio yanaweka akiba ya gesi nchini Tanzania kwa zaidi ya futi za ujazo trilioni 50. Serikali inadhani idadi hiyo inaweza kuongezeka maradufu wakati visima vya ziada vya uchunguzi vitakapochimbwa, na kuvifanya kuwa chanzo kikubwa cha mapato.

Kuna kapuni tanzu mbili zilizopo chini ya TPDC ambazo ni Gas Supply Company Limited (GASCO) na TANOIL Investments Limited.

**TPDC LAIMARIKA KIUCHUMI**

Kwa sasa TPDC limeimarika kifedha kwa kupata faida kila mwaka ambapo mwaka 2021/22 lilipata faida ya Sh bilioni 97.78 ukilinganisha na Sh bilioni 22.92 kwa mwaka 2020/21. Aidha mizania ya fedha imekuwa imara zaidi kutoka Sh trilioni 3.17 mwaka 2018/2019 hadi Sh trilioni 4.21 mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la Sh trilioni 1.042 katika kipindi cha miaka minne. Takwimu za mafanikio hayo zimetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC , Mussa M. Makame wakati akieleza mafanikio ya shirika katika utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema katika utekelezaji wa majukumu yake kadiri ya malengo ya kuanzishwa kwake, TPDC imekuwa na mafanikio makubwa yanayogawanyika katika maeneo sita.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni uhakika wa upatikanaji wa nishati , usambazaji wa nishati safi, mafanikio ya kiutendaji na kifedha, utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya Taifa,utekelezaji wa miradi na uwajibikaji kwa jamii.

Mwaka wa fedha 2021/22 Shirika lilifanikiwa kulipa Serikali Sh bilioni 62.84 katika Mfuko wa Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi, na kuipa gawio la Sh bilioni 2.7. Aidha, alisema Shirika limelipa kodi mbalimbali Sh bilioni 57.85 huku likiendelea kutekeleza dira yake ya kuwa Kampuni kubwa ya mafuta inayojiendesha kibiashara.






# NISHATI MBADALA ITAHARAKISHA KUFIKIA MALENGO'

**Hakuna shaka yeyote ndani ya kipindi kifupi falsafa yake hii imefanya kazi kwa kiwango kikubwa, Tanzania mpya**







Naipongeza serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiona haja ya kuelekeza nguvu zetu kwenye mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hii itasaidia kuokoa mamilioni ya miti kukatwa pamoja na kukoa afya za wanawake wengi mjini na vijijini.

NA JIMMY KIANGO

Dhana iliyojengeka kwa Watanzania wengi kwenye eneo la nishati safi ya kupikia ni kutumia gesi au umeme, nje ya hapa walio wengi hawaamini kingine chochote.

Fikra hizi zinaweza kubeba ukweli wa asilimia 51 tu na asilimia hizi zinaweza kuleta uhalisia kwenye nchi zilizoendelea si hizi zinazojikongoja katika maendeleo hasa za Afrika na Tanzania ikiwemo.

Ukweli ni kwamba kwenye nchi nyingi za Afrika bei ya umeme iko juu na hata upatikanaji wake si wa uhakika, kama hiyo haitoshi hata majiko yenyewe yanayopaswa kutumia nishati ya umeme nayo ni ghali.

Kama ilivyo kwenye umeme ndivyo ilivyo kwenye gesi, bei yake ni ghali, upatikanaji wake hasa vijijini ni mgumu, bado kiwango cha usambazaji ni kidogo na sababu kubwa ni gharama kubwa ya kusambaza mabomba yatakayoweza kusafirisha gesi asilia kwenye nyumba za watu.

Pamoja na changamoto hizo hapo juu za umeme na gesi, bado kuna suala la matumizi sahihi ya nishati hizo, wataalamu wa masuala ya nishati wanasema kuwa utumiaji usiozingatia matumizi sahihi na salama ni hatari kwa watumiaji.

Ikumbukwe kuwa maeneo mengi ya nchi yetu yanahusisha makazi holela ambayo hayajapimwa kabla ya watu kuanza makazi, maeneo mengi yamekutana na zoezi la kurasimisha na si kupima katika mpangilio sahihi, hali inayoongeza hatari ya kukosekana kwa matumizi bora na salama ya gesi.

Itakumbukwa kuwa mapema Mei 8,2024, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua mkakati wa matumizi ya Nishati safi ya kupikia.

Kimsingi ni mkakati wenye tija uliobeba dhamira ya kumuondoa mama wa mjini na kijijini kwenye hatari ya kudhurika na hewa ukaa inayotokana na kuni na mkaa. Utekelezaji wenye tija wa mkakati huu utasaidia kuepusha vifo 34,000 vya wakina mama vinavyotokana na matumizi ya kuni na mkaa kwa kila mwaka, pamoja na kuokoa zaidi ya hekta 400,000 za misitu kuteketezwa kila mwaka .

Kwenye hili Rais Samia ni mkombozi wa mwanamke jikoni na anastahili kuungwa mkono kama ambavyo yeye mwenyewe alivyofungua milango kwa sekta binafsi kushiriki moja kwa moja katika kulifanikisha hili kwa kuwekeza kwenye uuzaji wa nishati safi ya kupikia.

Hii maana yake nini? Maana yake serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi wahakikishe mkakati huo wa miaka 10 unafanikiwa kikamilifu kwa kufikia lengo la kufikia asilimia 80 ya Watanzania wote hadi kufikia mwaka 2034.

Hata hivyo changamoto zilizopo zinaweza kukwamisha mkakati huo kutekelezwa kwa wakati stahiki, hali iliyowaibua wadau kushauri namna sahihi ya kuyafikia malengo hayo kuwa ni vema tukaanza na nishati mbadala ambayo ni mkaa wa kutengeneza, majiko banifu na hata makaa ya mawe.

# #MTUE MAMA MZIGO WA KUNI



Mkuu wa Hifadhi ya Milima ya Udzungwa, Theodora Batiho, alimpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiona haja ya kumuondolea mwanamke adha jikoni.

Batiho anasema yeye yuko wilayani, anaijua adhana wanayopata wanawake kutokana na kutafuta niashati ya kupikia.

"Wanawake wengi hasa waliopo vijijini, wanapata tabu sana, kwanza wanahaingaika kutafuta hizo kuni, wanatembea umbali mrefu, wanaingia kwenye mapori na misitu kusaka kuni, huko wanakutana na adha mbalimbali wakiwemo wanyama wakali pamoja na nyoka.

"… lakini kama haitoshi wanaingia kwenye mapori ya akiba n ahata kwenye hifadhi za taifa hali inayowafanywa kukamatwa na askari wetu, hii ni adha kwao kwa sababu hairuhusiwi kuingia hifadhini bila ruhusa, lakini hawana namna wanalazimika kuingia kwa siri ili kusaka kuni na wakikamatwa ni tatizo, zote hizi ni changamoto.

"Hata hivyo uwezekano wa kuondokana na changamoto hizi upo, ni mkubwa sana, najua kuna gesi na mkaa ambavyo vinatajwa kuwa vyanzo vikuu vya nishati safi ya kupikia, lakini ukweli ni kwamba hivi vitu ni ghali na upatikanaji wake si wa uhakika kwenye maeneo mengi vijijini.

KAULI ZA WABUNGE

# nishati safi YA KUPIKIA

Katika kufanikisha hatua ya kumtumia mama mzigo wa kuni na kumuondoa kijana kwenye ukataji wa miti kwa ajili ya kukata miti, mwaka 2023 serikali iligawa mitungi 100 kwa wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kugawia wananchi kwenye majimbo yao.



***Jarida la TZ&BEYOND** liliwafikia baadhi ya wabunge ili kupata maoni yao juu ya mkakati huo wa serikali uliolenga kumtua mama mzigo wa kuni na kumuokolea muda ili kumpa nafasi ya kushiriki kwenye shughuli nyengine za kiuchumi.*



**FATMA TOUFIQ**
Viti Maalum mkoa wa Dodoma



**MERRY MASANJA**
Mbunge Viti Maalum mkoa wa Mwanza



**PROFESA JOYCE NDALICHAKO**
Mbunge wa Kasulu Mjini



**KHADIJA SHABANI TAYA 'KEYSHA'**
Mbunge Viti Maalum



**RIDHIWANI KIKWETE**
Mbunge wa Chalinze



**HAMIS TALETALE**
Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki

**FATMA TOUFIQ**
(VITI MAALUM MKOA WA DODOMA)
Anatamani kuona wanawake wajasiriamali wanakuwa chachu ya utunzaji wa mazingira kwa kuingia kwenye matumizi ya gesi kuliko kuendelea kuharibu mazingira kwa kutumia kuni na mkaa.

**PROFESA JOYCE NDALICHAKO**
(MBUNGE WA KASULU MJINI)
"Natamani kuona mama lishe na baba lishe wakiinuka kiuchumi na kupitia nishati hii ya gesi naamini itarahisisha kazi ya upikaji wa chakula kwa taasisi, nyumbani na kwa mamalishe na babalishe wote hatua itakayoongeza kipato chao,

**RIDHIWANI KIKWETE**
(MBUNGE WA CHALINZE)
"Lengo langu ni kuhakikisha mkakati wa nishati safi ya kupikia unafanikiwa kwa kiwango kikubwa kwenye jimbo lang una kwa nchi kwa ujumla, nataka kuona mwanamke anaondoka na adha ya kutafuta kuni kwa matumizi ya chakula.

**MERRY MASANJA**
(MBUNGE VITI MAALUM MKOA WA MWANZA)
"Mimi ni mama n ani mpishi pia, naamini mkakati huu wa nishati safi ya kupikia utasaidia kuwaokoa wamama wengi kutoka kwenye hatari ya kupata maradhi yanayosababishwa na nishati chafu kutoka kwenye kuni na mkaa.

**KHADIJA SHABANI TAYA 'KEYSHA'**
(MBUNGE VITI MAALUM)
"Namshuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali walemavu, amekuwa ni msaada mkubwa sana kwetu, hata hili suala la nishati safi ya kupikia ni mwendelezo wa kumsaidia mwanamke mwenye ulemavu."

**HAMIS TALETALE 'BABU TALE'**
(MBUNGE WA MOROGORO KUSINI MASHARIKI).
"Nimefurahishwa na uamuzi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kuiona haja ya kuja na mkakati huu wa nishati safi ya kupikia, hii itasaidia kupunguza vifo vya wakina mama vinavyotokana na moshi wa mkaa na kuni. "Nauunga mkono mkakati hu una nitahakikisha najitahidi kuufanikisha



**PATROBAS KATAMBI**
Mbunge Shinyanga Mjini



**COSTANTINE KANYASU**
Mbunge wa Geita Mjini,

**"NAMPONGEZA SANA RAIS SAMIA KWA HATUA YAKE HII YA KUIONA HAJA YA KUMUONDOLEA MADHILA MWANAMKE WA KIJIJINI NA NAAHIDI NITAFANYA KILA NIWEZACHO KULISAIDIA TAIFA LANGU KUYAFIKIA MALENGO YA ASILIMIA 80 KUHAKIKISHA WATANZANIA WENGI ZAIDI WANATUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA,"**

**PATROBAS KATAMBI**
(MBUNGE SHINYANGA MJINI)
"Najua lengo la serikali ni kumtua mama mzigo wa kuni na ili kulifanikisha hili, wote tunapaswa kuungana na serikali kutafuta namna sahihi ya kulifikia lengo hili kwa haraka, binafsi yangu najua madhara ya matumizi ya kuni, ninao ndugu zangu ambao wamekumbana na adha hii. Katimba ambae pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, amegawa majiko ya gesi 665 kwa wajasiriamali waliopo kwenye jimbo lake.

**COSTANTINE KANYASU**
MBUNGE WA GEITA MJINI,
Costantine Kanyasu amesema matumizi ya Nishati safi ya kupikia yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuwaondolea wakina mama adha ya maradhi yanayotokana na moshi wa kuni.

Alisema katika kuhakikisha agenda ya Rais Samis Suluhu Hassan inafikiwa amegawa majiko 200 kwa waapiga kura wake.

"Nimegawa majiko kwa akina mama, lakini pia nimebakiza majiko ambayo nitayagawa kwenye vijiwe 25 vya wauza kahawa wa hapa mjini Geita wakiwemo mama ntilie" Kanyasu amesema na kuongeza;

## MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA NI
# AGENDA
## MAHSUSI

DOTO BITEKO

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati



Matumizi ya nishati safi ya kupikia ni agenda mahususi ambayo imechukua nafasi kubwa katika Sera, mipango na mikakati ya serikali mbalimbali duniani.

Umuhimu wa agenda hii unasukumwa na ongezeko la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na athari za kiafya zinzotokana na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Lengo Namba 7 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa limejikita katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati nafuu, inayopatikana kwa urahisi, endelevu na ya kisasa kwa wote.

Hata hivyo bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa nishati nafuu, endelevu na za uhakika kwa ajili ya matumizi mbalimbali hususan ya kupikia hasa kwa nchi zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania.

Hali hii inasababisha wananchi wengi na baadhi ya taasisi kuendelea kutumia nishati isiyo safi ya kupikia, jambo linaloendelea kuchochea ongezeko la athari za kimazingira, kiafya, kiuchumi na kijamii.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikibuni na kutekeleza Sera na mikakati yenye lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na utunzaji wa mazingira.

Pamoja na utekelezaji wa Sera na mikakati hiyo chini ya sekta na taasisi mbalimbali, hakuna mwongozo wa Kitaifa unaotoa nishati safi ya kupikia na kuondokana na nishati chafu.

Kutokana na hali hii, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa Mjadala wa Kitaifa wa Nishati safi ya kupikia mwaka 2022 alielekeza kuangaliwa kwa Mkakati wa Taifa utakaotoa mwongozo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Kwa muktadha huo, serikali imeandaa mkakati wa taifa wa Matumizi ya nishati safi ya kupikia ambao unatoa mwelekeo wan chi wa kuhamia katika nishati safi ya kupikia.

Mkakati huo una lengo la kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Hivyo natumia fursa hii kutoa wito kwa wadau wote, zikiwemo Wizara za kisekta, Taasisi za umma, Idara za Serikali, Tawala za Miko ana serikali za Mitaa, asasi za kiraia, sekta binafsi, washirika wa maendeleo na umma kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mkakati huu.

Ni imani yangu kuwa ifikapo mwaka 2034 nchi yetu itakuwa imepiga hatua kubwa kayika kukuza kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia, hali itakayowezesha utunzaji wa mazingira, kuboresha afya na ustawi wa jamii, kukuza uchumi na kuchangia kufikiwa kwa Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030.

MTUE MA KUNI MA

# Afrika

## AFRIKA IWEKEZA KWENYE NISHATI SAFI YA KUPIKIA

NA MWANDISHI WETU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameitaka Afrika kuunga mkono agenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kumuokoa mwanamke na maradhi yanayotokana na moshi, lakini pia kumuondolea adha ya kupoteza muda mwingi kutafuta kuni.

Rais Dokta Samia, ametoa wito kwa viongozi wa Afrika kuhakikisha wanaipa kipaumbele agenda hiyo ambayo pia itasaidia kuharakisha maendeleo kwa nchi zao.

Alitoa wito huo kwenye mkutano uliowahusisha viongozi wa Afrika na Korea Kusini uliofanyika Jijini Seoul nchini Korea Kusini.

Rais Dokta Samia alisema wanawake wengi barani Afrika wanaathirika kutokana na matumizi ya nishati chafu ya kupikia na kusema umefika muda wa agenda hiyo kupewa kipaumbele cha kutosha kwa nchi zote za Afrika.

Pia aliutumia mkutano huo kutoa wito kwa nchi ya Korea Kusini kushirikiana na mataifa ya Afrika katika kuifanikisha agenda hiyo ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Rais Samia amesema, kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mkuu wa benki ya maendeleo ya Afrika AFDB Dr. Akinumwi Adesina wamehimiza jitihada za wadau wa Kimataifa kuchangia fedha ili kusaidia kusukuma mbele agenda ya matumizi ya nishati safi.

Mkutano huo ulifunguliwa Juni 4,2024 na Rais wa Korea Kusini Yoon Suk Yeol, ambapo mkutano huo ulihudhuriwa na marais mbalimbali wa Afrika, akiwemo William Ruto wa Kenya, Nana Akufo-Addo wa Ghana, Filipe Nyusi wa Msumbiji, Emmerson Mnangagwa wa Zimbabwe, Paul Kagame wa Rwanda na Mokgweetsi Masisi wa Botswana.



**80**

**Mkakati huo una lengo la kuhakikisha kuwa asilimia ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.**

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# MIFUMO YA HUDUMA BINAFSI KWA MWANACHAMA NA MWAJIRI

Mifumo hii ni ya mwajiri **"Employer Portal"** na mwanachama **"Member Portal"** inapatikana kupitia tovuti ya Mfuko **"www.nssf.or.tz"** bofya kifute cha **"Self Service"** (Huduma Binafsi).




- Mfumo wa **"Employer Portal"** ni maalum unaowawezesha waajiri kuangalia michango ya wafanyakazi wao, unaohamasisha uwazi na uwajibikaji kati ya Mfuko na mwajiri.
- Mfumo wa **"Member Portal"** unamuwezesha mwanachama kupata taarifa za michango yake.

@NssfTanzania









# TIPER

TANZANIA INTERNATIONAL PETROLEUM RESERVES L.T.D




TIPER
BULK STORAGE





**TIPER** the joint venture company between the government of Tanzania and Oryx Energies SA (OESA) based in Geneva with equal shares 50% each operates the largest storage facility for petroleum in the country. Current storage capacity is 253.7 million litres.

TIPER which used to be known as Tanzanian Italian Petroleum Refining (TIPER) Company Limited, commissioned refinery business in 1966. In year 2000, the refinery business ceased. In 1999 Agippetrol International (BV) - "Agip" sold its assets in TIPER as well as the 50% shareholding of the company to Oryx Energies SA., GENEVA (OESA). The remaining 50% shares continued to be owned by the Government of Tanzania.

Following the liberalization of the downstream petroleum subsector in Tanzania, TIPER found it uneconomical to operate as a refinery. In mid-2000, the company changed its main objective from refining to petroleum product storage. The refinery was decommissioned, scrapped and the plant was then converted in to a refined petroleum storage terminal, whose core business is the bulk storage and handling of refined petroleum products with delivery of the customer's product through cross pumping to other terminals, back-loading for onward transshipment and truck loading for onward sale at local commercial and retail outlets as well as for transit.






**TIPER** operating as a bulk liquid storage entity, stores low sulphur diesel (AGO), Premium Motor Spirit " (PMS), Dual Purpose Kerosene (DPK) and Heavy Fuel Oil (HFO 180) which is widely used in industrial applications. TIPER operating as storage facility has facilitated to a greater extent the availability of petroleum products in the country as well as for neighboring land locked countries.

## TIPER'S CURRENT STORAGE CAPACITY BY PRODUCT IS SHOWN BELOW:

| Product | Capacity (Litres) |
|---|---|
| Diesel (AGO) | 180,246,000 |
| Premium Motor Spirit " (PMS) | 56,302,000 |
| Dual Purpose Kerosene (DPK) | 5,723,000 |
| HFO 180 | 11,383,000 |
| Total Storage Capacity | 253,654,000 |



# TIPER's future plan include:

- To increase the capacity by adding more tankage to facilitate the envisaged opera tions of a special bonded warehouse and eventual Strategic Petroleum Reserve (SPR).
- Lifting the operating standards in all fronts especially the HSSEQ and attain the ISO certification.
- To gain validation in practical terms, to become the hub for petroleum supply chain for East and Southern Africa.
- Enhancing Truck Loading Operations to facilitate operational efficiency for Various customers.







# SHUKRANI

za dhati kwa WASHIRIKA WETU


KCB
BANK
Internet Banking
I-Bank
Agency Banking
ATM
Mobile Banking
Mobi
TISS
EFT
TT
E.A Payments
Government Electronics Payments (GEPG)
Let's talk
Internet Banking App
My experience with KCB Bank is that of modern times...